CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (**SUZA**)
Kichocheo cha Mabadiliko ya Jamii
Simu: 255 24 2233337 / 773333167
tovuti: www.suza.ac.tz barua pepe: vc@suza.ac.tz

THE STATE UNIVERSITY OF ZANZIBAR
P.O. BOX 146
ZANZIBAR
TANZANIA
SUZA

TANGAZO LA MAHAFALI YA 22

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kinawatangazia wahitimu wote wa mwaka wa masomo wa 2025/2026 wa Kampasi zote za SUZA pamoja na wananchi wote kwa jumla kwamba mahafali ya Ishirini na Mbili (22) ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar yatafanyika siku ya Jumamosi ya tarehe 19 Disemba, 2026 katika ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Kampasi ya Tunguu kuanzia 2:00 asubuhi.

Mazoezi ya mahafali (rehearsal) yatafanyika siku ya Alhamis, tarehe 17 Disemba 2026, kuanzia saa 2:00 asubuhi katika ukumbi Dkt. Ali Mohamed Shein. Wahitimu wote watakaoshiriki katika mahafali ni lazima washiriki katika mazoezi haya kwa siku na wakati uliotajwa.

Aidha, wahitimu watalazimika kuthibitisha ushiriki wao kuanzia siku ya Jumatatu, tarehe 07 Disemba 2026. Uthibitisho huo unatakiwa uambatane na malipo ya joho la mahafali kiasi cha TZS. 30,000 kwa kutumia *control number* ambayo inapatikana kupitia mfumo wa SUZIMS kwenye akaunti zao. Kwa wahitimu ambao wapo kwenye mfumo wa OSIM watapata *control number* kwa kupitia ***payment.suza.ac.tz***.

Majoho ya mahafali yatatolewa katika Kampasi ya Tunguu kuanzia siku ya Jumatatu, tarehe 14 Disemba 2026, kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 alasiri, na mwisho wa kuchukua joho utakuwa siku ya mazoezi ya mahafali. Wahitimu wanapaswa kurudisha majoho si zaidi ya tarehe 31 Disemba 2026. **Faini ya TZS. 5,000** itatozwa kwa atakayechelewa kurejesha joho baada ya tarehe ya mwisho. **Malipo ya Joho ni lazima kwa kila mhitimu.** Inasisitizwa kuwa wahitimu watajigharamia wenyewe gharama za chakula na malazi kwa kipindi chote cha maandalizi na mahafali.

Washiriki wote wa mahafali na waalikwa wanatakiwa wawe wameshakaa katika nafasi walizopangiwa ifikapo saa 1.30 asubuhi. Inasisitizwa kuwa mtu yoyote hataruhusiwa kuingia kwenye ukumbi wa mahafali baada ya kuingia kwa maandamano.

IMETOLEWA NA OFISI YA NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – TAALUMA, UTAFITI NA USHAURI ELEKEZI

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)